file — ~~Admission~~ join Instructions

SHULE YA SEKONDARI LUWAWASI,
S.L.P 583,
**SONGEA.**
Mob: 0768 – 300260/ 0787 – 245876
0673 – 852340/ 0752 – 985940

**Kumb. Na. MOEVT/LUWWS/A-3/3/.........**

Jina la Mwanafunzi

..........................................................................

..........................................................................

..........................................................................

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUWAWASI WILAYA YA SONGEA (M) MKOA WA RUVUMA MWAKA** 2020/2021

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu umechaguliwa kujiunga na Kidato cha Kwanza katika Shule hii mwaka 2019. Shule ya Sekondari Luwawasi ipo umbali wa km 2½ Magharibi mwa Halmashauri ya Songea Manispaa.

Usafiri wa basi kutoka Mjini mpaka Ruhuwiko unapatikana katika Kituo cha Mabasi cha Songea, nauli ni Tshs 400/=.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 07/01/2019 unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe 07/01/2019 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/01/2019 ndani ya siku saba.

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

### 2.1 SARE ZA SHULE

**Wasichana:-**

(i) Sketi marinda sita tu, sketi ndefu, iguse viatu ifike kwenye kifundo cha miguu (Itakaguliwa kikamilifu – fuata maelekezo)
(ii) Blauzi nyeupe mikono mifupi na tai ya kijani kibichi.
(iii) Viatu vyeusi vya kamba (visiwe na visigino virefu)
(iv) Soksi nyeupe
(v) Sweta la bluu

**Wavulana:-**

(i) Suruali rangi ya kijani
(ii) Shati jeupe mikono mifupi na tai ya kijani kibichi
(iii) Viatu vyeusi vya kamba
(iv) Soksi nyeusi
(v) Sweta la blue

**NB:** Suruali modo ya kubana marufuku na hairuhusiwi

## 2.2 SARE YA MICHEZO

Sare ya michezo kwa shule hii:-

(i) T – Shirt pea 1 rangi ya bluu kwa wavulana na bukta rangi ya bluu

(ii) T – Shirt pea 1 rangi ya bluu kwa wasichana na bukta rangi ya bluu

## 2.3 VIFAA VYA MASOMO

Daftari, Kalamu na Mkebe wa hesabu

## 2.4 USAFIRI MA MATIBABU

(i) Nauli ya kwenda shuleni na kurudi nyumbani pamoja na matibabu ni jukumu la mzazi/ mlezi

**NB:** Sare za shule na michezo zitakaguliwa kikamilifu siku ya kufungua shule.

## 2.5 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inatolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baara ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.

(c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation)

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na utakazopewa

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika Shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(h) Kuzingatia Ratiba ya Shule wakati wote

(i) Kutunza Mali za Umma.

**3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHA SHULE:-**

(a) Wizi
(b) Uasherati na Ushoga
(c) Ubakaji
(d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulenya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
(e) Kupigana au kupiga
(f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
(g) Kudharau Bendera ya Taifa
(h) Kuoa au kuolewa
(i) Kutoa mimba
(j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(k) Kukataa adhabu kwa makusudi
(l) Kuwa na Simu ya mkononi

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

(a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara atakaporipoti shuleni.
(b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
(c) Fomu ya Mzazi kukiri kukubaliana na Sheria, Kanuni na Maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**NB: Fomu "A" na "B" zijazwe na zirudishwe Shuleni siku unapomleta mtoto Shuleni Shule inapofunguliwa.**

**MOTTO WA SHULE**

***"ELIMU, NIDHAMU NA UFANISI"***

**JUMUIYA YA SHULE YA SEKONDARI LUWAWASI INAKUKARIBISHA SANA**

..........Msigwa

**MWL. V.Y. MSIGWA**
**MKUU WA SHULE**

LUWAWASI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 583
DATE 2020/2021
SONGEA

Fomu "A"

# GOVERNMENT OF TANZANIA
# REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

From:.........................................
.................................................
.................................................
.................................................
Date:...............................20.........

**Part A:**

To the Medical Officer,

...................................................

...................................................

Mr. / Mrs. / Miss.......................................................... (Name in full).

Please examine the above as to his/her physical and mental fitness for a full time Teacher Training / Secondary Education. The examination should include for the following Categories (I – III) each category or sub – category of which render the applicant ineligible in case of a defect.

1. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (d) Venereal diseases
   (e) Leprosy
   (f) Epilepsy

2. Neuroses

3. Other serious diseases

**Part B: Medical Certificate**
(To be completed by a Government Medical Officer)

I have examined the above named and consider that he is physically ft/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher/training/Secondary Education.

1. (a) Eye – sight...........................................................................
   (b) Hearing...............................................................................
   (c) Limbs..................................................................................
   (d) Venereal diseases.................................................................
   (e) Leprosy................................................................................
   (f) Epilepsy...............................................................................

2. Neuroses......................................................................................

3. Other serious diseases..................................................................

Date: ................................................ Signature:....................................

Station:.............................................. Designation:................................

LUWAWASI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 583
DATE 20/20/2024
SONGEA

**Fomu "B"**

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI

MKOA WA RUVUMA
0787 – 245876/ 0768 – 300260
0752 – 985940/ 0655 – 300261

SHULE YA SEKONDARI LUWAWASI,
S.L.P 583,
**SONGEA.**

***AHADI YA KUTEKELEZA WAJIBU***

Mimi ........................................................................... naikubali nafasi niliyoipata katika Shule ys Sekondari Luwawasi. Nafahamu kuwa nitasoma kwa faida yangu na Taifa kwa ujumla.

Naahidi mbele ya Mzazi/ Mlezi wangu kuwa nitajitahidi kwa upeo na uwezo wangu kuwa mwanafunzi mwema. Naahidi kuwa sitashiriki katika mambo yatakayosababisha wanafunzi kusimamishwa Shule.

Naahidi kuwa nitashirikiana na Walimu pamoja na wanafunzi wenzangu katika kila jambo lenye manufaa kwa Shule na Taifa kwa ujumla.

***SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI***

Mimi ........................................................................... nimesoma yote na kuyaelewa. Naahidi kwamba nitampatia mahitaji yote kama ilivyotajwa katika Fomu za kujiunga na Shule. Ripoti na barua zote zinazohusu mwanafunzi huu ziletwe kwangu kwa anuani hii:-

..............................................................................................

..............................................................................................

..............................................................................................

Jina na Sahihi ya Mzazi/ Mlezi ..................................................

..............................................................................................

Tarehe ........................................................................................

LUWAWASI SECONDARY SCHOOL
P.O.BOX 583
DATE 2020/2021
SONGEA